

Kuelewa na Kushiriki Hisia za Wengine

Tukio la 1

Gabi alikuwa akila chakula cha mchana pamoja na marafiki zake, lakini alipokwenda msalani, aliacha simu yake mezani. Alipokuwa huko, rafiki yake kwa jina Castel alichukua simu ya Gabi na kuanza kusoma ujumbe wake. Ujumbe wa kwanza aliouona ulikuwa ni wa mamake Gabi aliyekuwa ameghadhabika kwa vile Gabi alianguka hisabati.

- Je, hii ingemfanya Gabi ahisi vipi?
- Sababu gani ingempelekea Gabi kutotaka kuwaambia marafiki zake kuhusu matokeo yake mabaya?
- Je, hatua yake Castel ilikuwa sawa?
- Je, wale marafiki wengine waliokuwa wakila pamoja mezani wangehisi vipi kuhusu hatua za Castel?
- Unafirikia vipi kuhusu Castel? Je, hatua ya Castel ilikuwa yenye maadili? Je, unaweza kupenda kuwa marafiki na Castel?
 - Ungehisi vipi ikiwa mtu angekufanyia hivyo?
 - Je, ni jambo jema mtu akikuchunguza? Je, na iwapo ulikuwa na shauku kumhusu rafiki?

Tukio la 2

Rodrigo anazungumza na Caitlin bahati mbaya anateleza na kuanguka matopeni. Caitlin anafikiri Rodrigo anakaa vibaya sana na anampiga picha ilhali Rodrigo naye anacheka na kuonekana kufedheheka.

- Kwa nini Caitlin anaweza kuchapisha picha hiyo mtandaoni?
- Kwa nini Rodrigo ameudhika?
- Unadhani Rodrigo anapaswa kumwambia Caitlin nini?
- Ungehisi vipi ikiwa mtu angekupiga picha inayofedhehesha? Je, unaweza kupenda kuiona mtandaoni?
- Je hali hii ni tukio la uonevu?

Tukio la 3

Victoria ni mwanafunzi wa miaka 15 na ana kaka wawili, mama na marafiki wengi pamoja na wanafunzi wenza. Victoria na Merek wanasoma pamoja na wanafanya kazi pamoja katika mradi fulani wa somo la sayansi. Jana walifanya jaribio la sayansi na wakati kila mmoja alipokea matokeo yake, Merek aligundua kwamba Victoria alikuwa ameuadhika. Wiki iliyofuata Victoria hakufika shuleni kwa siku kadhaa hivyo Merek akalazimika kufanya mradi ule wa sayansi peke yake. Victoria aliporudi, akamwarifu Merek kwamba alilazimika kuenda kumwona daktari bila kusema chochote kingine.

- Je, nani anahitaji kufahamu kuhusu matokeo yake shuleni? Rekodi yake ya kimatibabu? Kwa nini?
- Je, Victoria angependa kuzungumza na nani kuhusu suala lolote lile?
- Maishani mwako, ni mifano ipi ya maelezo ambayo ungetaka wazazi wako / watunzaji wako waone wala sio marafiki au vinginevyo?

Kuelewa na Kushiriki Hisia za Wengine: Nakala ya Mwalimu

Tukio la 1

Gabi alikuwa akila chakula cha mchana pamoja na marafiki zake, lakini alipokwenda msalani, aliacha simu yake mezani. Alipokuwa huko, rafiki yake kwa jina Castel alichukua simu ya Gabi na kuanza kusoma ujumbe wake. Ujumbe wa kwanza aliouona ulikuwa ni wa mamake Gabi aliyekuwa ameghadhabika kwa vile Gabi alianguka hisabati.

- Je, hii ingemfanya Gabi ahisi vipi?
 - Gabi anaweza kuhisi kwamba faragha yake imekiukwa na anaweza kupoteza Imani kwa rafiki yake.
- Sababu gani ingempelekea Gabi kutotaka kuwaambia marafiki zake kuhusu matokeo yake mabaya?
 - Gabi anaweza kuhisi kwamba alama zake ni maelezo ya faragha.
- Je, hatua yake Castel ilikuwa sawa?
 - Washiriki wanapaswa kuzingatia tabia zao binafsi kuhusiana na faragha ya alama na simu zao pamoja na matarajio yao kwa marafiki zao.
- Je, wale marafiki wengine waliokuwa wakila pamoja mezani wangehisi vipi kuhusu hatua za Castel?
 - Washiriki wanapaswa kuzingatia hatua ambayo wangechukua ikiwa waliona tabia inayoweza kuwa si njema.
- Unafirikia vipi kuhusu Castel? Je, hatua ya Castel ilikuwa yenye maadili? Je, unaweza kupenda kuwa marafiki na Castel?
 - Ungehisi vipi ikiwa mtu angekufanyia hivyo?
 - Je, ni jambo jema mtu akikuchunguza? Je, na iwapo ulikuwa na shauku kumhusu rafiki?
 - Washiriki wanapaswa kutafakari kuhusu tabia zao binafsi kuhusiana na faragha na mahusiano ya kibinafsi.

Tukio la 2

Rodrigo anazungumza na Caitlin bahati mbaya anateleza na kuanguka matopeni. Caitlin anafikiri Rodrigo anakaa vibaya sana na anampiga picha ilhali Rodrigo naye anacheka na kuonekana kufedheheka.

- Kwa nini Caitlin anaweza kuchapisha picha hiyo mtandaoni?

- Washiriki wanapaswa kutambua vichochezi vya Caitlin: kuwachekesha watu au watu kupenda picha huwa ni njia moja inayokubalika inayochochea mtu kuchapisha jambo mtandaoni, ilimradi kufanya hivo hakutamdhuru mtu mwingine.

- Kwa nini Rodrigo ameudhika?

- Washiriki wanapaswa kutafaraki kuhusu jinsi ya kuzingatia hisia za watu wengine wakati wakitumia mitandao ya kijamii.

- Unadhani Rodrigo anapaswa kumwambia Caitlin nini?

- Washiriki wanapaswa kubuni mikakati ya kushughulikia tabia hii.

- Ungehisi vipi ikiwa mtu angekupiga picha inayofedhehesha? Je, unaweza kupenda kuiona mtandaoni?

- Washiriki wanapaswa kuzingatia tabia zao binafsi kuhusiana na kile ambacho wangependa kishirikiwe mtandaoni na wengine.

- Je hali hii ni tukio la uonevu?

- Washiriki wanapaswa kuzingatia aina ya matendo ya uonevu na wajadili vipengele vya hali hii mahususi.

Tukio la 3

Victoria ni mwanafunzi wa miaka 15 na ana kaka wawili, mama na marafiki wengi pamoja na wanafunzi wenza. Victoria na Marek wanasoma pamoja na wanafanya kazi pamoja katika mradi fulani wa somo la sayansi. Jana walifanya jaribio la sayansi na wakati kila mmoja alipokea matokeo yake, Marek aligundua kwamba Victoria alikuwa ameudhika. Wiki iliyofuata Victoria hakufika shuleni kwa siku kadhaa hivyo Marek akalazimika kufanya mradi ule wa sayansi peke yake. Victoria aliporudi, akamwarifu Marek kwamba alilazimika kuenda kumwona daktari bila kusema chochote kingine.

- Je, nani anahitaji kufahamu kuhusu matokeo yake shuleni? Rekodi yake ya kimatibabu? Kwa nini?

- Washiriki wanapaswa kuzingatia jinsi maelezo tofauti yanavyokuwa na viwango tofauti vya faragha. Matokeo ya Victoria pale shuleni ni maelezo

nyeti ambayo hangelipenda marafiki zake, watu anaosoma pamoja nao au umma kwa jumla kufahamu. Hata hivyo, maelezo hayo sio siri kwa wazazi / watunzaji wake. Hali hii ni saa na rekodi yake ya kimatibabu, ingawa maelezo haya ni nyeti zaidi.

- Je, Victoria angependa kuzungumza na nani kuhusu suala lolote lile?

- Huenda Victoria mwenyewe angependa kuweka maelezo yake kuwa faragha. Uamuzi huu unapaswa kuheshimiwa. Anaweza kuchagua kushiriki baadhi wala sio maelezo yote ya faragha. Kwa mfano, anaweza kushiriki na wazazi/watunzaji wake kuhusu panda shuka zake za matokeo pale shuleni lakini hawezi kushiriki na marafiki zake.

- Maishani mwako, ni mifano ipi ya maelezo ambayo ungetaka wazazi wako / watunzaji wako waone wala sio marafiki au vinginevyo?

- Washiriki wanapaswa kuzingatia chaguo zao binafsi kuhusiana na faragha.